Jina ........................................................................Nambari ya Mtahiniwa...................................

Sahihi ya mtahiniwa...........................................Nambari ya Usajili……………………………..

Shule………………………………………………Tarehe....................................................

# BUNAMFAN CLUSTER EXAMINATIONS 2021

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**Karatasi ya 3**
**Muda: Saa 2½**
**DESEMBA**

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali **manne** pekee.*
*(d) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*
*(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
*(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*
*(g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(h) Majibu yote **sharti** yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **Sehemu** | **A** | **B** | | **C** | | **D** | | **E** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Swali** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** |
| **Alama** | | | | | | | | |

## SEHEMU YA A: TAMTHILILA

*(Kigogo – Pauline Kea)*

1. Swali la lazima.

a) ‘’Yaani umenonaje wewe? Waona mimi ni ganda la muwa la juzi.’’

i. Eleza muktadha wa dondo hili. (al. 4)

ii. Tambua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (al. 2)

iii. Fafanua jinsi wahusika walivyogeuzwa ganda la muwa katika tamthilia. (al. 6)

b) ‘’ Niko tayari kuwaweka pahali pao mmoja baada ya mwingine.’’ ‘’… Wamesahau vipi wasilolijua?’’

Eleza umuhimu wa matumizi ya mbinu rejeshi ukirejelea dondoo hili. (al. 12)

access more freepast papers on the website www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA B: RIWAYA

*(Chozi la Heri – Assumpta Matei)*

*Jibu swali la 2 au 3*

2. a) Baba, umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusimama dede?’’

i. Eleza jazanda iliyotumika katika dondoo hili. (al. 2)

ii. Thibitisha kuwa mtoto anayerejelewa hajasota wala kusimama dede.(al. 8)

b)Eleza umuhimu wa mazungumzo baina ya Tila na Ridhaa. (al. 10)

3. i) Eleza umuhimu wa barua aliyoiandika Bwana Kalima kwa Lunga. (al. 10)

ii) Soma kifungu hiki kisha ujibu swali.

> Mkuu wa shule, walimu na wanafunzi wenzangu, swala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumeona jinsi misitu imevamiwa na viongozi wenye mate ya fisi. Nasikia baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali ya umma wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kuwapoka makazi yao. Maelfu ya maekari ya misitu yamefyekwa na kujengwa viwanda. Badala ya mibambakofi na miti mingine inayosafisha hewa, michai imetwa nafasi yake. Wanaohusika na matendo haya wanapoulizwa hudai kuwa michai si adui wa mazingira! Wengine wanasema kwamba misitu haina budi kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula. La kuhuzunisha ni kwamba hawa hawa wanaosema hivyo ndio wanakita majengo ya kifahari katika maeneo yanyofaa

kutengewa upanzi wa chakula! Wengine wamediriki kunyakua hata madhababu kwenye Mlima wa Nasibu ili kujenga hoteli kubwa za kitalii. Wazee wetu hawana hata pahali pa kuchomea kafara! Tunakata miti bila kupanda mingine. Tazameni shuleni humu! Hata mabustani ya maua tunashindwa kuyastwisha! Tukiendelea hivyo, bila shaka sehemu sehemu yetu itakuwa jangwa!

Fafanua maudhui yoyote kumi yanayojitokeza katika dondoo hili. (al. 10)

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

access more free pastpapers on this website www.freekcsepastpapers.com

*Jibu swali la 4 au 5*

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Sikilizeni wimbo huu:
Niliokuwa mtoto nilitwa chacha
Kwa matamshi yangu ya sasa
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure.

Huu utakuwa wimbo wako Utakapostaafu
urudipo nyumbani Umelewa kangara na
nyayo zako
Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini.
Utakuwa kichekesho cha watoto Watakaoukuita,
Ticha! Popote upitapo.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu, Mijusi
watataga mayai ndani ya viatu Vyako
vilivyokwisha visiginino.
Na ndani ya sidiria chakavu
Zilizoshikizwa Kamba kwa pini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu Za
marashi na za bia.

Na manyigu yatajenga ndani ya kofia
Zilizosahaulika kutani
Utakapokufa nge watazaliana Chini
ya jiwe juu ya kaburi lako, Na mlevi
fulani akipita atapenga

Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke
Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

Lakini wakati ungali hai
Unaweza kubadilisha mkondo wa maji Lakini
kwanza mzungumze. Wewe na mimi. Acha
mioyo yote izungumzwe
Baada ya kunyanyaswa Na
kisha nusu mshahara.

Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi?
Utafundisha tena ngonjera?
Utapeleka tena wanafunzi asubuhi
Wakajipange barabarani kusubiri Mgeni
afikaye saa kumi na apitapo
Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe Na
huku nyuma mwasambaa na njaa?
Tazama hilo runda madaftari mezani
Utalimaliza kwa mshahara mkia wa mbuzi?
Tuzungumze. Ninyi na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze
Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo
Mtawekwa kwenye vijiti na kutupwa Nje ya
ua, ndani mtawaacha
Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya

Sikilizeni walimu,
Anzeni kufundisha hesabu mpya
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini Ni
sawa na sifuri. Hapana utawala Fundisheni
historia historia mpya
Hapo zamani za sasa
Hapakuwa na serikali.

Sikilizeni kwa makini
Umoja hatuna
Twasambaratika kama nyumba
Tulicho nacho ni woga,
Na kinachotuangusha ni unafiki. Lakini
tusikate tamaa kama mbuni. Tukiupata
umoja bado tunayo silaha. Kura.

access more free pastpapers on this website www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Fafanua sifa za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. (al. 5)

(b) Eleza jinsi maudhui ya utamaushi yanavyojitokeza ukimrejelea nafsi-nenewa. (al. 4)

(c) Nafsi-nenewa anapaswa kujilaumu kwa masaibu yake. Thibitisha. (al. 2)

(d) (i) Bainisha nafsi-neni katika shairi hili. (al. 1)

(ii) Taja toni ya shairi hili. Toa mfano. (al. 2)

(e) Eleza matumizi mawili mawili ya usambamba na jazanda katika shiri hili.(al. 4)

(f) Eleza maana ya kufungu kifuatacho:

Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri. (al. 2)

**5. soma shairi kisha ujibu maswali.**

Leo ‘mekuita,
Kwa upole nitanena,
Tabiya hii yako mwana

Uli wa kulaza damu,
Pahala nawe hudumu,
Hutufai nawe humu,

Wapendani naumi,
Hulimi na walimi
Haya sijaona mimi,

Mwiza kazi yu wa chira
Asiyeta ajira
Ndiye muja wa hasara,

Unavitaka vya bure
Lako ndizo hamurere
Uchao ‘wa ‘tuza bure.

La mno lako ni ung’are
Uturi ujirashire
Hukosi kuzua ghere

Nikupe ya moyo
“Kayatiye masikiyo
Si yetu tujuwapo

Na uzembe uzidiyo
Uchaoni mbiyombiyo
Na hiyo shambiroyo

Uniizia gange
wataka ukajitenge
Nakuasa ujichunge

Ni andewaye tenge
Wala hashiki shilange
Hubomoa asijenge

Hulitoa jasho lako
Umebaki mitiko
Sizo zetu nyendo zako

Uzirembe nyele zako
Ukatembee kwa deko
Na marashi ya mnuko

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com

Unazani utaoa?
Jasho nalo hujatoa,
Utaithibiti ndoa?

Unafaa kujitoa,
Na mali ukayazoa,
Ndipo utapopoa

Si mambo ya kutanga,
Chunga utajikaanga
Mchumba chumbiya mwenga

Utafanyani kiwatunga
Na hilo likawe janga,
Mwanangu hutochenga

Kisomo ndiyo unayo,
Ujuzi unao kocho,
Upate ukitakacho

Mwana wa ‘ntiya kichocho
Umekuwa kitumiwacho
Unawapa wapendacho

Komu mwanangu ukome
Usombombi uukome,
Sitakwita te’niseme

Ukware si kuwa dume
Wa itaha ndiye dume
Muungwana ja kimeme

Mradi unayo masikizi
Kazituwe nyendo hizi,
Ukasuhubiye kazi,

Nakoma zaidi s’ezi
Nimekuweko na juzi,
Nimejizolea ujuzi,

Utamwoa wa nani?
Utachokishika nini?
Wa kukubali nani?

Fanye kazi kwa manani
Hamadi i kibindoni
Ukamtafute mwendani

Fi na huhu fi na yule
Umetujile uwele
Na yule ukamuole

Himila wakahimile
Na lije likulemele
Na wote wakikujile

Shahada umejitwaliya
hutaki kuutumiya
Kile cha kukufaiya

Kwona umejiachiya
Kidhani wawatumiya
Na wanachokutakiya

Usinifishe mveyeleo
Ukome kwanzia leo
Ishapita hii leo

Dume ni ajira
Anakheshimu nafseo
Fikira nokwelezeo

Haya umenisikiya
Ukawe wa kutuliya
Halafu itakufaiya

Yametosha mekwambiya
Miyaka menipitiya
Na ndiyo ha ‘nakupa haya

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Fafanua sifa za kiarudhi za shairi hili. (al. 3)
b) Kando na kigezo cha idadi ya mishororo, chambua bahari nyingine tatu za shairi hili. (al. 3)
c) Huku ukitolea mifano mwafaka, fafanua mambo mawili aliyofanya mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (al. 2)
d) Andika ubeti wa nane kwa mtindo tutumbi. (al. 3)
e) Tambua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa na mshairi. (al. 2)
f) Eleza dhamira ya shairi hili. (al. 1)
g) Tambua nafsi-nenewa katika shairi hili. (al. 1)
h) Ni nini toni ya shairi hili? Eleza. (al. 2)
i) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama iliyotumika katika shairi hili. (al. 2)
   (i) ghere
   (ii) sitaha

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

*(Tumbo Lisilodhiba na Hadithi nyingine –A. Chokocho na D. Kayanda)*

*Jibu swali la 6 au 7*

6. ‘’Dunia we’ duinia. Dunia ya mwenye nguvu, si ya mimi dhaifu wa nguvu. Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi.’’

a) Thibitisha jinsi dunia ilivyokuwa msumari moto juu ya donda bichi kwa mhusika katika dondoo hili. (al. 10)
b) Eleza jinsi maudhui ya ushirikina ulivyojitokeza katika hadithi ya Tulipokutana Tena. (al. 10)

**7. Shibe Inatumaliza**

a) ‘’Mh! Ati kama mimi. Kwani wewe umekula nini?’’
‘’Mimi? Hata sikutazama. Nimekomba tu. Wewe je?’’

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
b) Tambua mbinu zozote mbili za uandishi zilizotumika katika dondoo hili. (al. 2)
c) Eleza jinsi wahusika mbali mbali walivyokomba rasilimali bila kutazama. (al. 8)
d) Tambua umuhimu wa DJ katika hadithi ya Shibe Inatumaliza. (al. 6)

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Wekamaya ndiye aliyemuumba binadamu wa kwanza akamwita Omwami. Jina hili Wekamaya alipewa kwa sababu wanajamii wa Omukwasi waliamini yeye ni mungu mwenye wema. Kwa sababu hii, siku moja alipokuwa akitembea katika bustani yake, Wekamaya alijiambia, ‘’Singependa Omwami wangu wawe wakifa kabisa, nataka afufuke.’’

Wakamaya alikuwa na wake wawili, Shiswitswi na Ngoitsi. Katika ndoa yao, Wamukaya aliweza kungamua kuwa Ngoitsi alikuwa mke aliyependa kutia chumvi katika maneno na hata kusema kinyume ya aliyoambiwa. Pia, alikuwa kigeugeu kama kinyonga. Kwa upande mwingine, Shiswitswi alikuwa mwadilifu na aliyejawa na busara kedekede. Alikuwa mkweli.

Wamukaya alipoona kuwa wakati umefika wa kumpasha Omwami habari ya uzima, alimwita mkewe Shiswitswi na kumwambia, ‘’Nenda bustanini na umwambie Omwami kuwa atakayekufa atafufuka.’’ Shiswitswi akaiitika na kusema, ‘’Ndio Wakamaya!’’ Katika harakati hizi, kumbe Ngoitsi alikuwa kasikia alivyotumwa Shiswitsi. Akajiambia mwenyewe, siwezi kugeuzwa ganda la muwa, ujumbe huu ntaipeleka mimi, ndiyo Omwami aniheshimu. Kwa kuwaza, akakumbuka udhaifu wa mke-mwenza wake ambao ulikuwa kuwa mpole. Akala yamini kuutumia.

Shiswitswi alianza safari na kuwaaga kwenda kwa bustani. Akatembea, akatembea, akatembeaaaaa! Alipofika baada ya siku mbili alishangaa kumpata Ngoitsi tayari bustanini. Tayari keshampa Omwami ujumbe, ‘’Wamukaya amesema kwamba watakokufa wataangamia milele’’ na Omwami kwa mshutuko tayari alishatoweka kutoka bustanini kwa kilio.

Na huu ndio mwisho wa hadithi yangu.

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com

**<u>Maswali</u>**

a) Tambua kipera hiki cha hadithi. (al. 2)

b) Kwa nini mtambaji anatumia maneno ‘’Na huu ndio mwisho wa hadithi yangu.’’ (al.4)

c) Tambua sifa zozote sita za kimtindo zinazojitokeza katika hadithi hii. (al. 6)

d) Fafanua njia zozote nne ambazo unaweza kutumia kukusanya data kuhusu kipera hiki. (al. 6)

e) Eleza njia zozote nne zinazoweza kutumika katika jamii ya kisasa kuendeleza kipera hiki. (al. 4)

access more free past papers on this website www.freekcsepastpapers.com